BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tisa – Tarehe 25 Septemba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

19. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Katika kukabiliana na changamoto nyingi zinazokikabili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi hasa katika eneo la kiwanja cha ndege kilichopo Nungwi, kuna umuhimu mkubwa wa kukipatia kiwanja cha ndege hicho angalau gari mbili za kuzimia moto, ili kukabiliana ipasavyo na tatizo la moto pale litakapotokezea.

    (a) Ni lini Serikali itapeleka gari la zimamoto angalau moja katika kiwanja cha ndege cha Nungwi.

    (b) Ni lini kiwanja cha ndege cha Nungwi kitaanza kuchukua abiria japo kwa ndege ndogo kupeleka Pemba, Dar es Salaam au angalau kwa kuanzia kwa kuwapeleka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Karume.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

47. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Kilima cha Nyarugusu ni kivuko muhimu kinachowasaidia wananchi kupita wao na mali zao kwa urahisi na takriban kwa kipindi kirefu sasa, wananchi wanapita kwa shida huku watendaji wa Mfuko wa Barabara wakija na kuweka ahadi na kurudi bila ya kuzitimiza.

    (a) Je, Serikali haioni kwa vile muda umekuwa mrefu, sasa ni

wakati muafaka kukikarabati kilima cha Nyarugusu.

(b) Je, watendaji wa Mfuko wa Barabara hawaoni kwamba kuwapa tena wananchi hao ahadi isiyotimilika ni kuwazidishia usumbufu wa kuvuka eneo hilo tegemezi.

113. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ibara ya 103(b) ya Ilani Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeelekeza kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza kupitia matumizi mabaya ya Teknolojia mpya ya Kidigitali.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutimiza maelekezo haya.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

35. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Nchi yetu imejaaliwa miti mingi ya aina mbali mbali inayotoa maua yenye kuvutia, tiba na haiba.

(a) Je, kuna aina ngapi adimu za miti ya maua.

(b) Kwa kuwa maua ni uwekezaji unaoingiza fedha za kigeni, Je, ni changamoto gani zinazopelekea kusiwe na uwekezaji wa mashamba ya maua.

**Wizara ya Afya:**

4. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Bomani ni kituo ambacho husaidia wananchi wengi katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar na hasa ukizingatia kuwa kituo hicho kinatoa huduma nzuri kwa wagonjwa wanaofika kituoni hapo.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inafahamu idadi ya wagonjwa wanaofika kituoni hapo na ni kubwa kiasi gani

ukilinganisha na ukubwa wa jengo lenyewe.

(b) Je, lini Serikali itafanya mazungumzo na Uongozi wa Jeshi la Polisi Zanzibar ili kukiimarisha kituo hicho katika majengo yake kwa vile majengo hayo ni ya kizamani na yana ufinyu wa nafasi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

53. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) limepewa jukumu la kisheria la kusimamia masuala yote yanayohusu lugha ya Kiswahili na kusimamia matumizi na maendeleo yake lakini pia kuhakikisha kuwa lugha hiyo inafanikiwa kukuwa na kuondosha changamoto zinazokikabili.

Je, BAKIZA inachukua mikakati ipi ya kuhakikisha kwamba mabadiliko mengi na kasi ya sayansi na teknolojia yanayotokea duniani hayaiathiri vibaya lugha yetu adhimu ya Kiswahili.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

38. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwa na makumbusho yatakayoonesha kazi mbali mbali za uvumbuzi na ubunifu zinazofanywa na wahitimu kutoka vyuo vikuu vya hapa Zanzibar.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**25 Septemba, 2023.** **KATIBU WA BARAZA.**